Kijarida cha Taarifa

Novemba 2013

# Misitu yetu inasimamiwaje?

## Wananchi wanena kuhusu usimamizi wa misitu Tanzania

## Utangulizi:

*Asasi za kiraia nchini Tanzania zimekubaliana kwamba changamoto kubwa zinazo ikabili sekta ya misitu katika ngazi zote zinahusiana na usimamizi wa rasilimali hizi. Makubaliano haya yalifikiwa katika Jukwaa la majadiliano la "Hali ya Usimamizi wa Misitu Tanzania – Maoni na mtazamo wa Wananchi" ambalo pia lilikuwa kama kichochea msingi cha kuleta mwelekeo bora wa kampeni ya wananchi kuokoa misitu yetu. Jukwaa la majadiliano la siku moja lilitoa fursa kwa wanajamii kushuhudia mbele ya jopo la wataalam wa misitu - viongozi wa serikali, wawakilishi wa Asazi za Kiraia, wafanyabiashara na Wabia wa Maendeleo - kushirikishana mawazo na masuala ya wananchi na kuona matumaini yao ya uzalishaji endelevu wa sekta ya misitu katika Tanzania. Baada ya kuwasikiliza mashuhuda, changamoto zilijadiliwa katika mdahalo, jambo ambalo lilisaidia kuyaleta masuala ya wananchi ngazi ya jamii kwenye ajenda za ngazi ya kitaifa.*

## Ujumbe Muhimu:

☞ **Tunahitaji kuboresha mawasiliano na elimu kuhusu haki na wajibu wa jamii.**

- Karibu shuhuda zote ziligusia kuendelea kukosekana kwa elimu kuhusu sera na sheria za misitu katika ngazi ya kijiji. Kukosekana kwa elimu kuliathiri shauku ya wanakijiji ya kusimamia misitu katika vijiji vya Kisarawe na Wilaya ya Kibaha.
- Kampeni ya Mama Misitu ilikuwa muhimu katika kuongeza uelewa wa wanakijiji juu ya haki na wajibu wao. Kuongezeka kwa uelewa kulimwezesha Diwani wa Kata ya Masaki kuhamasisha vyema wapiga kura wake kusimamia misitu.
- Elimu ya sheria ya misitu ilibadilisha mtazamo wa jamii kuhusu misitu, kwa kuiona kama rasilimali ambayo wao wenyewe wanapaswa waisimamie na kuilinda badala ya kuisubiri serikali ifanye hivyo.

☞ **Utaratibu wa kugawana mafao ya misitu bado hautekelezwi ipasavyo**

- Wanakijiji wa kijiji cha Kipangege kinachopakana na Msitu wa Hifadhi wa Ruvu Kusini waliendelea kulinda msitu huo bila mkataba wa maandishi ambao unawahakikishia manufaa na haki zao.
- Kukosekana kwa mkataba wa maandishi kuna maana kwamba mpango wa kuchangia gharama na kugawana mafao ulikuwa hautumiki kikamilifu, hali iliyo sababisha wanakijiji kupoteza imani katika zoezi la Usimamizi wa Pamoja wa Misitu kabla kampeni ya Mama Misitu kuanza.
- Katika kijiji cha Kisangani wanakijiji walikuwa wakifanya doria misituni, lakini walitishiwa na maafisa wa polisi ambao hawakuheshimu makubaliano ya Mkataba wa Usimamizi wa Pamoja wa Misitu kati ya jamii na Wakala wa Misitu wa serikali (TFS).

☞ **Utekelezaji wa mifumo ya kisheria iliyopo ikiwa ni pamoja na kufungua mashitaka haifanyiki kwa utaratibu mzuri**

- o Katika kijiji cha Kisangani mamlaka ya doria ya msitu wa kijiji haikutambulika na polisi na kusababisha bughudha na vitisho.

- o Maafisa wa polisi ambao walitumia vibaya madaraka yao kwa kuwatishia wana-doria wa msitu wa kijiji cha Kisangani hawakuchukuliwa hatua stahiki za kisheria, hali iliyowaacha wanakijiji wakiwa na wasiwasi na kukatishwa tamaa.

☞ **Ni lazima kuchukua hatua kwenye kuzuia rushwa, biashara haramu ya misitu na ushirikiano kati ya mamlaka na watendaji wasiokuwa waaminifu ili kuboresha usimamizi wa misitu**

- o Mazao haramu ya misitu yaliyo kamatwa katika doria ya msitu wa kijiji cha Kisangani, baadaye yaliachiliwa na maafisa wa polisi wasiokuwa waadilifu waliokuwa wakitishia silaha.
- o Ushirikiano kati ya mamlaka na watu wanaojishughulisha na shughuli haramu za misitu ulidhoofisha juhudi za wanakijiji kusimamia vizuri Hifadhi ya Msitu wa Ruvu Kusini.
- o Maafisa wa jeshi la polisi wenye silaha na wala rushwa walipelekea wanakijiji wasiokuwa na silaha kuhofia usalama wao wakati wa kufanya doria ya msitu.

☞ **Ushiriki wa Jamii na Sekta Binafsi unahitaji kuimarishwa zaidi**

- o Mwakilishi wa wafanyabiashara wa mbao alisisitiza umuhimu wa kushirikisha sekta binafsi katika jitihada za kusimamia misitu kama vile kuongeza ufanisi katika uvunaji wa misitu.
- o Ushiriki wa jamii na sekta binafsi katika usimamizi wa misitu utapelekea kila kundi la wadau kufuatilia shughuli za makundi mengine.

**Tunahitaji kuboresha na kurahisisha miongozo ili wadau waweze kuelewa vyema majukumu yao**

- Mwakilishi wa wafanyabiashara wa mbao wa sekta binafsi alionesha hisia kwamba miongozo ambayo ni vigumu sana kuielewa na kuitekeleza ni sababu mojawapo inayofanya shughuli haramu ziendelee.
- Wito ulitolewa wa kuhusisha wadau wote wakati serikali inapokuwa inaandaa kanuni na miongozo yoyote inayohusu usimamizi wa misitu.
- Kuna haja ya kuwa na Kanuni za Maadili kwa ajili ya wafanyakazi wa serikali, sekta binafsi na jamii zitakazotekelezwa.

**Kuna umuhimu mkubwa wa kuendeleza, kuimarisha na kukuza Uzalishaji wa kipato mbadala na Makampuni yanayo jishughulisha na Misitu**

- o Makampuni yanayojishughulisha na biashara halali za mazao ya Misitu ni muhimu yaendelee kuwepo ili jamii iweze kunufaika kutokana na uandaaji na usindikaji na kuongeza thamani ya rasilimali za misitu
- o Usimamizi wa Misitu ni kitu muhimu sana katika kuwezesha upatikanaji wa makampuni yanayofanya biashara endelevu za misitu.
- o Umiliki salama, huduma za ugani na upatikanaji wa masoko pia ni muhimu katika kuhakikisha makampuni yanayofanya biashara endelevu ya misitu yadumu.

## Shuhuda:

Dhima kuu ya Jukwaa la majadiliano kuhusu Usimamizi wa Misitu ilikuwa ni kusikia shuhuda kutoka kwa wanakijiji na viongozi wa jamii ambako kampeni ya Mama Misitu ilitembelea. Mama Misitu ni kampeni ya mawasiliano yenye lengo la kuboresha usimamizi wa misitu ya Tanzania na kupunguza uvunaji haramu wa misitu, ili watanzania waweze kunufaika zaidi na misitu endelevu inayosimamiwa vyema. Maelezo ya kina kuhusu kampeni hii yanaweza kupatikana hapa - http://www.mamamisitu.org/.

Ndani ya chapisho hili kumbukumbu ya shuhuda za wanajamii ambao walishuhudia biashara ya misitu kama inavyofanyika Tanzania. Ni vyema kutambua kwamba mwakilishi wa sekta binafsi ya wafanyabiashara wa mbao na chama cha wajasiriamali, ambaye alikuwa amealikwa kushuhudia, alipatwa na woga kutokana na hali ya majadiliano, baadaye alikataa kuzungumza wakati wa kipindi cha shuhuda.

**Bw. Shomari Juma-Mwenyekiti wa Halmashauri ya Kijiji cha Kipangege (Wilaya ya Kibaha)**

- o *"Tulidhani ilikuwa ni wajibu wa serikali kulinda misitu na siyo wajibu wetu, kitu ambacho kilisababisha rasilimali za misitu kutoweka. Kwa hiyo, baada ya kupokea elimu kuhusu usimamizi endelevu wa misitu na matumizi ya rasilimali za msitu. Tuliandaa mpango wa usimamizi wa msitu na sheria ndogo ya kulinda misitu. Awali ilionekana kama majaribio kwani hatukuwa na mkataba rasmi na serikali. Tulikuwa na wasiwasi juu ya jinsi gani tutalinda haki zetu, kwani hapakuwa na mkataba wa maandishi kati yetu na serikali. Hata hivyo, tulinufaika kwa kulipwa asilimia ishirini ya thamani ya mbao haramu zilizopokonywa kwa watu. Aidha tulinufaika na*

*rasilimali za misitu kama vile uyoga na mimea ya dawa. Sasa ni wakati muafaka wa kuwa na mkataba wa kisheria kati ya jamii zetu na Wakala wa Misitu (TFS), utakaofanya pande zote mbili kutambua gharama, mafao, haki na wajibu."*

**Bw. Subira Juma-Katibu wa mtandao wa MJUMITA (SHIWAMARU - Shirikisho la Watetezi wa Mazingira Ruvu) Wilaya ya Kibaha**

*…"Kampeni ya Mama Misitu imekuwa ya manufaa sana kwa sababu sasa naelewa vyema kuhusu majukumu na usimamizi bora wa misitu. Sasa tumekuwa na uwezo wa kuitisha mkutano na kuwawajibisha baadhi ya wajumbe wa Kamati ya Mazingira ya Kijiji. Tumekuwa na uwezo wa kuihoji Halmashauri ya Kijiji kuhusu mapato na matumizi yanayohusiana na misitu. Halmashauri ya Kijiji yenyewe kwa sasa imeomba kupata taarifa mpya kutoka kwenye kamati kuhusu shughuli zao na ripoti hii itawasilishwa kwenye mkutano ujao wa kijiji".*

**Bi. Pili Kondo Chamguhi – Diwani wa Kata ya Masaki, Wilaya ya Kisarawe**

*"Ninasema ukweli kabisa kwamba tangu kampeni ya Mama Misitu ilipoanza kumekuwa na mabadiliko makubwa, kwa sasa jamii inashiriki kikamilifu katika kulinda misitu yao. Kwa hiyo naunga mkono kampeni ya Mama Misitu kwa asilimia mia moja na niko tayari wakati wowote kushirikiana na wadau katika shughuli yoyote. Pia naomba kwamba elimu hii itolewe kwa madiwani wote katika maeneo yao kwani wao ni wawakilishi wazuri sana na wahamasishaji wa watu".*

**Bw. Mwinyi Saidi Ali - Mwanakijiji kutoka kijiji cha Kisangani, Kata ya Masaki, Wilaya ya Kisarawe**

*…"Naomba kueleza tukio moja lililo tokea wakati mimi na wenzangu tulikuwa tukifanya doria katika msitu ambako tulikutana na watu wakipakua tanuri la mkaa haramu. Wakati tulipokuwa tunahojiana nao askari polisi wawili walitokea na mmoja wao alikuwa na bunduki. Walianza kuongea nasi kwa jazba na uadui mkubwa, wakituuliza tulikuwa tunafanya nini msituni. Tuliwaeleza kwamba tulikuwa katika doria ya msitu, huku tukiwaonesha vitambulisho vyetu lakini badala yake walitushutumu kuwa ni majangili na kwamba hatupaswi kufanya shughuli yoyote msituni. Tulitoa taarifa ya tukio hilo kwa Mkuu wa Polisi wa Wilaya, na kuwataja maafisa wa polisi wawili wanaohusika. Mkuu wa polisi aliahidi kufuatilia suala hilo na baadaye tuligundua kwamba wote walipewa karipio kali. Kwa kuwa tulikuwa tunakabiliana na chombo cha dola tuliamua kukubali kile tulichoambiwa lakini tulibaki na hofu kubwa kwa sababu wale maafisa wa polisi wangeweza kutudhuru wakati wowote, kama wangetaka kufanya hivyo. Bado tunawaona Kisarawe wote wawili mara kwa mara".*

## Majibu ya washiriki na mjadala wa jumla:

*Kongamano la Usimamizi wa Misitu ni tukio lililohudhuriwa na jopo la wataalam wa misitu ambao walikusanywa ili kutoa shuhuda zao. Jopo lilikuwa na watu kama Bw. Valentine Msusa kutoka idara ya misitu serikali kuu, Wakala wa Misitu Tanzania (TFS); Bw. Ben Sulus Katibu Mtendaji wa Chama kikubwa zaidi Tanzania cha viwanda vya mbao, kinachojulikana kwa kifupi SHIVIMITA; Bw. Abdallah Ulega Gala ambaye ni Mkuu wa Wilaya, cheo cha juu kabisa katika Wilaya ya Kilwa ambako ni moja ya eneo linaloongoza kwa uvunaji wa misitu Tanzania; na Bi Inger Naess Mshauri wa Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi katika Ubalozi wa Norway, mmoja ya wabia wa maendeleo ya Tanzania kwa miaka mingi, na hutoa msaada kwa sekta ya misitu.*

**Bw.Valentine Msusa-Mkurugenzi wa Mipango na Matumizi ya Rasilimali, Wakala wa Misitu Tanzania (TFS)**

*TFS kwa sasa inaandaa kanuni ili kufikia mwezi Julai 2013 ugawanaji wa mafao uweze kuratibiwa kisheria. TFS kwa sasa inapanga kupeleka Ma meneja Misitu kila wilaya na kila msitu wa hifadhi. Wasimamizi hawa wa Msitu watakuwa na wajibu wa kuhamasisha usimamizi shirikishi wa Misitu (PFM). Bw. Msusa alikiri kwamba watu wengi wanaojihusisha na biashara haramu ya misitu ni wafanyakazi wa serikali, ikiwa ni pamoja na askari. Bw. Msusa alitambua kwamba polisi na vyombo vingine vya dola vinaweza kuwa tatizo. Aliahidi kuwa TFS siku zote itasaidia jamii.*

**Bw. Ben Sulus-Katibu Mtendaji SHIVIMITA**

*Bw.Sulus alieleza kuwa ingawa Waziri Mkuu amezitaka idara zote za serikali kununua samani zao kutoka vyanzo vya Tanzania, hata hivyo, viwanda vya samani vya hapa nchini vimekuwa wakikabiliwa na ugumu katika kupata malighafi. Bw.Sulus aliitaka TFS kusisitiza zaidi juu ya kuongeza ufanisi katika uvunaji misitu na usindikaji, kwa kuboresha viwango vya ahueni katika uvunaji wa mbao na katika uchomaji mkaa. Bw.Sulus alitoa wito wa kuwa na Kanuni za Maadili miongoni mwa sekta binafsi. Bw.Sulus alidai kuwa baadhi ya matatizo katika utekelezaji wa sheria ya misitu ni kwamba miongozo ya sasa ni duni. Alipendekeza kuwa miongozo ya baadaye iandaliwe katika mchakato shirikishi na iwe rahisi, lugha rafiki kwa mtumiaji (iwe kiswahili) itumike katika nyaraka zote zilizokusudiwa kwa matumizi ya umma.*

**Bw.Abdallah Ulega Gala-Mkuu wa Wilaya,Wilaya ya Kilwa, Lindi**

*Bw.Ulega alihisi kuwa wakazi wa Ukanda wa Pwani wamekuwa wahanga wa muda mrefu wa usimamizi mbovu wa misitu. Bw.Ulega alibainisha kwamba alikuwa akiwaona watu wakibeba magunia ya mkaa kupeleka Dar lakini alihisi kwamba, hakukuwa na maendeleo yanayowapata njia mbadala za kujipatia kipato. Bw.Ulega alisema kuwa kuna haja ya kuhamasisha matumizi ya njia mbadala ya kuzalisha mkaa. Mkuu wa Wilaya alieleza kuwa Kijiji cha Nanjirinji kilipata shilingi milioni 50 za kitanzania kutokana na mauzo ya mbao nyeusi za mpingo wa Afrika Sound Fair N ; ambayo yalikuwa yakiwezeshwa na Asasi ya Kiraia ya Mkakati wa Maendeleo na Kuhifadhi Mpingo (Mpingo Conservation and Development Initiative-MCDI). Wadau wanapaswa kutafuta njia za kuiwezesha jamii kwa kutembelea na kupima misitu ya hifadhi ili jamii iweze kumiliki idadi kubwa ya misitu. Mkuu wa Wilaya aliwataarifu washiriki kwamba amepiga marufuku uvunaji wa mbao katika Wilaya ya Kilwa na kubainisha kuwa magogo ni vigumu zaidi kuyasafirisha kuliko mbao, kwa hiyo, huenda ni bora kuwataka wafanyabiashara kusafirisha magogo badala ya mbao na hivyo kupunguza biashara haramu ya mbao.*

**Inger Naess - Mshauri, Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi, Ubalozi wa Norway**

*Bi Naess aliona kwamba usimamizi ni tatizo kubwa katika misitu ambalo limesababisha misitu kuendelea kutoweka. Bi Naess alionyesha kukatishwa tamaa kwamba kulikuwa na ukosefu wa utashi kwa upande wa serikali, kwani 90% ya fedha kwa ajili ya misitu zilitoka kwa wafadhili. Bi Naess aliwakumbusha wajumbe kuwa kuna haja ya kushughulikia kikamilifu vyanzo vya uharibifu wa misitu kutokana na ukataji mitu uliokithiri. Kuna haja pia ya kuwa na shughuli mbadala za kuzalisha mapato kwa wananchi na suala la kugawana mafao ni la muhimu sana kushughulikiwa.*

**Simon Milledge - IIED:**

*Bw. Milledge alisisitiza umuhimu wa mafao kwa wananchi, kwa kuuliza ni biashara gani ya misitu inayoweza kuboresha maisha ya jamii (kwa mfano; uuzaji vijishamba vya miti, ufugaji wa nyuki au uchomaji mkaa endelevu). Ilielezwa kwamba mambo 4 ni muhimu ili kuwa na biashara endelevu ya misitu, yaani 1) Umiliki - kwa kurahisisha mchakato wa umiliki uwe nafuu, na wa haraka; 2) Masoko – kurahisisha ubadilishanaji wa bidhaa na huduma; 3) Ugani - kwa kufanya upatikanaji wa taarifa uwe rahisi, na 4) Uwakilishi –sauti ya wadau kwenye majukwaa ya kufanya maamuzi.*

## Mapendekezo:

1. Mapendekezo kwa TNRF kuandaa kongamano la wadau wa sekta binafsi tu, ili kuhakikisha sauti zao zinasikika, ingawa unyeti wao lazima uzingatiwe.

2. Mapendekezo kwa TNRF na wabia walioko Tanzania kufuatilia na kusaidia katika kukamilisha, kupitisha na kuingiza Kanuni za Maadili.

3. Mapendekezo kwa TNRF kufuatilia mazungumzo na serikali ili kupima ahadi za TFS kwa kuzipangia muda wa utekelezaji na ili ziweze kufuatilika na kuwajibishana

4. Mapendekezo kwa TNRF kuchunguza mbinu za kutoa msaada kwa jamii ili kuandaa maandiko mradi yanayoweza kufadhiliwa na kuyawasilisha TFF ili kupewa fedha.

5. Mapendekezo kwa TNRF kupitia MCDI, ambayo Mkuu wa Wilaya alizungumzia sana, kutathmini ufanisi na athari ya kupiga marufuku usafirishaji wa mbao huko Kilwa

6. Mapendekezo kwa TNRF na wabia wake kutafiti namna bora ya kuonesha mafanikio katika Wilaya ya Kilwa katika suala la kupatia kijiji mapato kutokana na mauzo halali na endelevu ya mbao, hasa uhusiano kati ya juhudi za kuboresha usimamizi wa ndani na jitihada za kuunda makampuni ya biashara ya misitu, kwani maeneo haya wakati mwingine hutengwa wakati wa majadiliano ya ki-sera.

7. Mapendekezo kwa TNRF na TFWG kufikiria kufanyia kazi masuala kama vile ya usalama wa umiliki, vigezo muafaka vya soko na kuwa na ujumuishaji ama au uwakilishi.

8. Mapendekezo kwa TNRF na wadau wake kuandaa ratiba ndani ya mpango wa kazi kwa ajili ya mchakato huu. Kwa ajili ya mchakato wa kutekeleza haya